HOWARD CENTER

Help is here.

KUADHIMISHA MIAKA 160

KITABU CHA MAELEKEZO CHA MTEJA

TOLEO LA SABA

SWAHILI

REJELEO LA HARAKA

Nambari Kuu Ya Howard Center

802-488-6000

Nambari ya Kufikia na Kuchukuliwa

Inapatikana Jumatatu – Ijumaa,
Saa 8:30 asubuhi hadi Saa 5:00 jioni

Mtu yeyote anaweza kupigia simu Howard Center. Tutatoa msaada, tuyajibu maswali, na tukuunganishe na rasilimali na huduma katika Howard Center au katika jamii.

Sababu za mara kwa mara za kupiga simu:

- Kutafuta tiba au ushauri nasaha
- Kuhisi wasiwasi kuhusu mtoto
- Kwa kuihitaji msaada kwa familia yako
- Kupata usaidizi wa kuwezeshwa kuishi maisha ya kawaida

First Call for Chittenden County

802-488-7777

Nambari ya Simu ya Dharura

Inapatikana 24/7/365

Sababu za mara kwa mara za kupiga simu:

- Hisia zilizozidi
- Mawazo ya kujiua
- Kusikia sauti zinazosumbua
- Wasiwasi kuhusu ustawi wa mpendwa wako

Sanaa ya jalada imechorwa na Howard Center Arts Collective. Msanii kiongozi: Eliza Roberts; Wasanii wasaidizi: Pamela Champagne, Anna Marie Mattson, Bernie Greene, Jens Arts, Edward Burke, Jordan Earle, Randy Pikul, Ivan Cruz, na wasanii wasioonyesha utambulisho wao kutoka Westview House, Pathways Vermont, na Lakeview House.

Huduma ya Dharura ya Afya ya Akili
802-488-MHUC (6482)

Huduma ya Dharura ya Afya ya Akili Isiyohitaji Miadi ya Howard Center

Inapatikana Jumatatu – Ijumaa,
Saa 8:30 asubuhi hadi Saa 5:00 jioni

Sababu zinazowafanya watu kutembelea kituo hiki sana:

- Msaada wa afya ya akili
- Msaada wa wanarika
- Utunzaji wa kuzuia kujiua
- Usimamizi wa utunzaji
- Tathmini na utunzaji wa kimatibabu unaohusiana

IN PARTNERSHIP WITH: The University of Vermont Medical Center; Community Health Centers; Pathways Vermont; Vermont Agency of Human Services Department of Mental Health

ORODHA YA YALIYOMO

KUHUSU HOWARD CENTER **UKURASA**

Rejeleo la Haraka 2
Karibu. 5
Ujumbe Wetu 6
Vile Tunavyosaidia. 6
Maono Yetu. 6
Maadili ya Msingi 6
Saa za Kufanya kazi 7

HUDUMA

Jinsi ya Kupata Usaidizi 8
Muundo wa Shirika. 9
Mchango wa Mtumiaji 9
Kulipia Huduma 10
Kujenga Mazingira Salama 11
Njia ya Utunzaji wa Ziada (Care Pathway) 14

HAKI ZA MTEJA NA TAARIFA YA KISHERIA

Usiri wa Taarifa 15
Haki za Wateja na Familia 16
Wajibu wa Wateja na Familia. 19
Muhtasari wa Kanuni za Maadili 20
Malalamiko ya Mtumiaji, na Sera ya Rufaa na Taratibu 22
Ofisi ya Udhibiti wa Kitaaluma – Mwenendo na Mchakato wa Malalamiko 24
Fomu ya Ushauri kwa Mteja 26
Ushirikishaji wa Jamii na Upangaji wa Mipango . . . 27

KUHUSU HOWARD CENTER

KARIBU!

Karibu Howard Center. Kwa miaka 160, shirika letu limetoa huduma na msaada bora kwa jamii yetu. Tunashukuru kwa fursa hio ya kukusaidia wewe na/au wapendwa wako.

Kitabu hiki cha mwongozo kinatoa muhtasari mfupi wa huduma mbalimbali za Howard Center, pamoja na maadili ya shirika letu, ambayo yanalenga kutoa huduma zinazomlenga mteja kwa watoto, vijana, watu wazima na familia. Lengo letu ni kutoa huduma za utunzaji na matibabu zinazomjali mteja, za heshima, na zenye ufanisi.

Kitabu hiki cha mwongozo kinaeleza taarifa muhimu kuhusu jinsi ya kuwasiliana na Howard Center ili kupokea huduma na haki na wajibu wako kama mteja. Kinapatikana katika lugha kadhaa tofauti, kwa maandishi makubwa na miundo ya kielektroniki. Ikiwa ungependa muundo tofauti au ikiwa unahitaji taarifa yoyote kuelezewa kikamilifu, tafadhali muulize mfanyakazi au piga simu kwa nambari yetu kuu kwa 802-488-6000.

Kwa niaba ya familia yetu ya Howard Center, tunatumai kuwa utapata huduma zetu kuwa za manufaa katika kukusaidia wewe na/au familia yako. Tunashukuru kwa fursa hii ya kufanya kazi na wewe, na tunatarajia kukusaidia katika safari yako ya ustawi.

Kwa Dhati,

Beth Holden, MS, LCMHC, LADC
Afisa Mkuu wa Huduma kwa Wateja

UJUMBE WETU

Tunawasaidia watu na jamii kustawi kwa kutoa msaada na huduma ili kushughulikia afya ya kiakili, matumizi ya madawa, na mahitaji ya kimaendeleo.

JINSI TUNAVYOSAIDIA

Howard Center kina historia kubwa kama mtoaji huduma anayeaminika katika jamii yetu. Kikiwa na urithi ulio na zaidi ya miaka 160, Howard Center kimekuwa kikitoa uendelezo, huruma, utunzaji wa hali ya juu, msaada, na matibabu kwa wale wanajamii walio na mahitaji. Kikiwa kilianzishwa mwaka wa 1865 kama shirika la kuhudumia watoto wa watu maskini, Howard Center sasa hivi kinatoa huduma za afya ya kiakili, matumizi ya madawa, na ya kimaendeleo kwa maisha yote.

Wafanyakazi wetu 1,500 hutoa usaidizi na msaada katika maeneo zaidi ya 60 katika kaunti nne. Zaidi ya wateja 19,000 na wanajamii walitugeukia mwaka uliopita kwa ajili ya usaidizi ili kuishi maisha yenye afya zaidi na yenye kutimiza zaidi.

MAONO YETU

Howard Center kimeongoza kitaifa katika utoaji wa misaada inayojumuisha na isiyo na mpaka iliyo na msingi wa jamii kwa watu, familia, na jamii zinazohitaji msaada. **Usaidizi uko hapa.**

MAADILI YA MSINGI

- Wateja wako katika mioyo yetu tunapofanya maamuzi.
- Sisi tumejitolea kwa ustawi na mafanikio ya mtu na watu wote kwa ujumla.
- Sisi ni wasimamizi wanaowajibika kwa rasilimali tulizopewa.
- Sisi tuko imara katika vitendo vyetu na kutafuta ubora.

Howard Center imejitolea katika afya na usalama wa wateja, wafanyakazi, na jamii yetu. Tafadhali muulize mhudumu wako au mpokeaji kuhusu tahadhari za usalama zilizopo sasa. Tafadhali kaa nyumbani ikiwa wewe ni mgonjwa au ikiwa una dalili za ugonjwa. Ikiwa unahitaji kufuta miadi yako, tunakuomba utuambie mapema iwezekanavyo. Miadi ya huduma za afya za kielektronoki zinapatikana kwa ombi.

SAA ZA KAZI ZA HOWARD CENTER

Ingawa baadhi ya vituo vinaweza kufunguliwa mapema au kuchelewa kufungwa, vituo vikuu vya Howard Center vitafunguliwa angalau kati ya saa 8:30 asubuhi na saa 4:00 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa, bila kujumuisha likizo za shirika.

VITUO VIKUU NI PAMOJA NA:

- 102 South Winooski Ave., Burlington, VT 05401
- 1138 Pine St., Burlington, VT 05401
- 172 Fairfield St., Saint Albans, VT 05478
- 208 Flynn Ave., Suite 3J, Burlington, VT 05401
- 300 Flynn Ave., Burlington, VT 05401
- 855 Pine St., Burlington, VT 05401
- 75 San Remo Dr., South Burlington, VT 05403
- 45 Clarke St., Burlington, VT 05401

HUDUMA

JINSI YA KUPATA USAIDIZI

Mtu yeyote anaweza kupiga simu kwa nambari kuu ya Howard Center, ambayo ni **802-488-6000**, ili kupata usaidizi. Utakapopiga simu, utaulizwa sababu yako ya kupiga simu, na huenda ukapokea taarifa kuhusu rasilimali za jamii na mahitaji ya ustahiki kwa mpango kadhaa. Kama inahitajika na inatakikana, utawekwa kwenye ratiba ya utathmini wa kuchukuliwa.

Mpango wa Huduma Itembeayo ya Mzozo ya Howard Center ya 24/7/365, Kupiga simu Haraka kwa Kaunti ya Chittenden, ipo kwa msaada kupitia kwa simu, uingilaji kati wa uso kwa uso, na utathmini wa mzozo. Kama uko nje ya Kaunti ya Chittenden na unahitaji msaada wa mzozo, tutakuunganisha na rasilimali katika eneo lako, kwa vile kila Kaunti katika Vermont iko na huduma yake ya mzozo.

Baada ya kuchukuliwa au tathmini ya mzozo, huenda ukapendekezwa kwa Programu moja au zaidi ya Howard Center au katika rasilimali nyingine za jamii, kama unavyohitajika. Mara kwa mara, rufaa hutolewa moja kwa moja kwa mpango wa Howard Center bila kuwa na tathmini ya mwanzo, kama vile wakati tunapopokea rufaa kutoka shuleni. Kama kuna orodha ya kungojea huduma inayohitajika, utapokea msaada ukiwa ungali unangojea. Pindi huduma za Howard Center zinapoanza, utapewa mtoaji huduma wa msingi ambaye atafanya kazi nawe kubaini mahitaji yako na mapendeleo. Kwa pamoja mtatengeneza mpangilio uliobinafsishwa wa huduma au mpangilio wa matibabu. Mtoaji wako wa huduma anaweza kufanya mapendekezo ya ziada, ndani ya Howard Center au kwa makundi mengine ya kijamii kama huduma zingine au msaada zinahitajika kwa ajili yako au wanafamilia.

Huduma ya ukalimani wa moja kwa moja unapatikana kwa njia za kupiga simu, ana kwa ana, na huduma za kimatibabu za njia za kielektroki.

Vermont 2-1-1 ni rasilimali ya jimbo yote inayotoa taarifa na mapendekezo kwa mkusanyiko wa huduma, zikiwemo ajira, masomo, huduma za utunzaji wa watoto, mipango ya serikali, makundi ya misaada, usaidizi wa kisheria, usafiri, rafu za chakula za jamii na rasilimali nyingine. Huduma hii ipo 24/7/365 na ni ya

kupiga simu kwa eneo kutoka kokote katika Vermont. Utafsiri wa lugha wa moja kwa moja unatolewa.

MUUNDO WA SHIRIKA

Howard Center kinatoa huduma kadhaa:

- Huduma za Kufikia na Kuchukuliwa
- Mipango ya mizozo
- Huduma za kupunguza madhara
- Mipango ya Nyumbani na za Jamii
- Huduma za Msaada za Muda Mrefu
- Dawa za ugonjwa unaotokana na matumizi ya opioidi
- Huduma za Wagonjwa wasiolazwa
- Mipango ya Shule

MCHANGO WA MTUMIAJI

Kuhusika kwako katika upangaji na tathmini ya huduma unazozipokea ni sehemu muhimu ya falsafa ya shirika hili. Kuna njia kadhaa ambazo tutahimiza kushiriki kwako.

Wateja wote na wanafamilia, ikiwa inafaa na imeruhusiwa na mteja, hushiriki katika uundaji wa mpango (mipango) yao ya huduma. Kabla ya huduma kuanza, utakutana na mtoaji huduma kwa ajili ya utathmini na kwa pamoja mtafanya maamuzi kuhusu ni huduma ipi inafaa kwako. Mtoaji huduma wa msingi atakabidhiwa kazi kwako. Kulingana na mpango(mipango), mtu huyu huenda akaitwa mshauri, mfanyakazi wa kijamii, mtaalamu, msimamizi wa utunzaji, mfanyakazi msaidizi, daktari, mwuguzi, au mtaalamu mwingine sawa na hawa. Mtoaji huyu wa huduma ataratibu huduma yako pamoja nawe. Wewe na Mtoaji wako wa huduma mtatengeneza mpangilio wa huduma yako ili kukidhi mahitaji yako ya kibinafsi. Utaamua ni nini ndio malengo yako, hatua gani unazozihitaji kuchukua ili kufikia malengo hayo, na vile utakavyojua kuwa uko tayari kupokea huduma nyingine au kuondoka kutoka kwa shirika. Mtoaji huduma wako atakusaidia kwa kukutuma ili upate huduma nyingine na/au kukutuma kwa wasjhriki wengine wa huduma ikiwa inahitajika. Mara nyingine, wateja huenda wakachagua kuitengeneza mipangilio spesheli mapema kwani huenda hali yao ikakuwa mbaya zaidi au wakapatwa na shida nyingine mbaya zaidi ambayo itafanya vigumu kwao kufanya maamuzi. Hizi zinaitwa vielekezo vya mapema. Ikiwa ungependa

mwelekezo wa mapema kuhusu matibabu, tafadhali muulize mtoa huduma wako.

Howard Center kina vikundi kadhaa, viitwavyo Kamati za Kudumu, kwa ajili ya wateja na/au familia zao kutoa maoni kuhusu huduma na mchango wao kwa kazi yetu ya sasa hivi na mwelekeo wa siku za usoni wa Howard Center. Kamati za Kudumu ni pamoja na: **Baraza la Ushauri wa Familia, Mfumo wa Utetezi wa Watumiaji, Kamati ya Kudumu ya Huduma za Maendeleo, na Kamati ya Ushauri ya Huduma za Matumizi** ya **Dawa za Kulevya**. Ongea na mtoaji wako wa huduma au uwasiliane kwa nambari kuu ya Howard Center, **802-488-6000**, kwa taarifa zaidi. Isitoshe, zaidi ya 50% ya Bodi ya Wadhamini ya Howard Center ni wateja au wanafamilia wa watu wanaopokea huduma.

Moja ya njia tunazozitumia kutathmini huduma zetu ni kuuliza vile wateja walivyoridhika na kama huduma hizo walizozipokea zimewasaidia. Tunatumia dodoso wakati ambapo wateja wanapokea huduma na kuwasiliana na wateja baada ya kutamatisha huduma. Kushiriki kwako katika mchakato huu ni kwa hiari na kunathaminiwa pakubwa.

KULIPIA HUDUMA

Huduma za Howard Center zinalipiwa kupitia njia kadhaa za vyanzo vya ufadhili.

Aina nyingi za bima, ikiwemo Medicaid, zinakubalika. Kama uko na bima, tafadhali ilete kadi yako kwa ziara yako ya kwanza. Kama uko na bima, tafadhali ilete kadi yako kwa ziara yako ya kwanza, pamoja na Kitambulisho chako kilicho na picha yako. Kama hauna bima, tutatumia kipimo kinachosonga ili kuweka malipo ya kibinafsi kulingana na hali yako ya kifedha. Tafadhali kumbuka kwamba iwapo utachagua kutoitumia bima yako, malipo ya kipimo kinachosonga hayawezi kutumika. Malipo yako utayaelezwa kabla ya kuanza kupokea huduma.

Howard Center kimejitolea kufanya kazi na wateja, familia, watoaji bima ya afya, mashirika ya eneo na jimbo, taasisi za kibinafsi, na vyanzo vingine ili kupata ufadhili ili kutoa msaada kwa huduma zinazohitajika. Upungufu wa kifedha hautapunguza upatikanaji wa huduma.

Kama una maswali kuhusu malipo, piga simu kwa 802-488-6920.

KUJENGA MAZINGIRA SALAMA

Kila eneo la Howard Center imewekwa vifaa vya kuzima moto na vya huduma ya kwanza. Kuna maelekezo ya kutorokea wakati wa dharura ambayo yamebandikwa karibu na kila mlango. Kila eneo lina mpangilio maalum wa uokoaji. Kama ungetaka nakala ya mpangilio wa dharura wa eneo, tafadhali muombe mtoaji wako wa huduma. Mazoezi ya kuzima moto na itifaki ya vizuizi vya usalama (pia vimebandikwa karibu na kila mlango) yanafanywa mara kwa mara.

Kwa kawaida, kuna angalau mhudumu moja kwa kila eneo ambaye amefundishwa kuhusu CPR na huduma ya kwanza. Wahudumu pia wamefundishwa kuhusu Tahadhari za Jumla. Ikiwa hali itatokea ambapo mtu anahitaji uangalizi wa kimatibau au ambapo Tahadhari za Jumla zitatekelezwa, mteja anaweza kuomba mfanyikazi kuingilia kati. Maeneo kadhaa yako na vifaa vya nje vya kudhibiti moyo za kujiendesha zenyewe.

Uhusiano wetu na wale tunaowahudumia umewekwa kwa misingi ya heshima ya pamoja na kufikiriana. Ingawa baadhi ya sheria na matarajio tunayoangazia huenda yakawekwa na jimbo au na kanuni za shirikisho, lengo letu kuu ni kuhakikisha kwamba wateja wetu wanapitia mambo mazuri.

Tabia ya kuheshimiana kwa pamoja inatarajiwa kutoka kwa wateja na wafanyakazi. Hakuna silaha zimekubaliwa katika mali ya shirika. Umiliki na/au matumizi ya moja au dawa zote haramu katika mali ya shirika umepigwa marufuku. Kulingana na sheria za jimbo la Vermont, matumizi ya bidhaa zote za tumbaku katika maeneo ya shirika, yote ndani na nje, umepigwa marufuku isipokuwa katika maeneo maalum ya baadhi ya makazi ya mipango yetu. “Bidhaa za Tumbaku” zinajumuisha, sigara za kielektroniki, na bidhaa au kifaa chochote cha nikotini ambacho hakijaidhinishwa na FDA. (Matumizi ya bidhaa za mbadala za nikotini zilizoidhinishwa na FDA kwa madhumuni ya kukomesha matumizi yameruhusiwa.) Kama ungetaka taarifa zaidi kuhusu takwimu za matumizi ya tumbaku, usaidizi wa kukomesha matumizi, au kuongea na mtaalumu wa kukomesha matumizi, tafadhali tembelea **www.802quits.org** au piga simu **1-800-784-8669**. Kwa raslimali zaidi za matibabu ya matumizi ya madawa, wasiliana na mtoaji huduma wako au utupigie simu namba ni **802-488-6000**.

Wanyama wa kuhudumia, wanyama wa kutoa msaada wa kihisia/marafiki, na wanyama wa kuhudumia wanaofundishwa wamekaribishwa katika mali ya shirika na katika shughuli mingi za shirika, kwani wafanyikazi wengi na wateja hushirikiana na wanyama wa kuhudumia. Ni muhimu kukumbuka kwamba ingawa wanyama wa kuhudumia na wanyama wa kuhudumia wanaofundishwa wameruhusiwa katika sehemu za makazi ya umma, wanyama wa msaada wa kihisia/marafiki hawana chaguo kama hilo ya kuyafikia kisheria. Tembelea www.ada.gov kwa sheria na kanuni kuhusu wanyama wa kuhudumia na wanyama wa msaada wa kihisia/marafiki.

Kulingana na Sheria ya Wamarekani walio na Ulemavu (ADA), mnyama wa kuhudumia ameelezewa kama "Mbwa ambaye amefundishwa kibinafsi kufanya kazi au kutekeleza jukumu kwa niaba ya mtu aliye na ulemavu. Wanyama wa kuhudumia walio katika mafundisho, wanaruhusiwa chini ya sheria ya ufikiaji ya Vermont. Wanyama wa kuhudumia huja kwa aina zote na kimo na hawaitaji kuwa wanaweza kutambuliwa kwa kuonekana. Wanafaa kuwa chini ya udhibiti wa mshikaji na wawe kwa kamba wakati wote isipokuwa kama kumfunga mnyama kunaathiri mshikaji anayesaidiwa kwa shughuli linalohusiana na ulemavu.

Mara kwa mara, huenda ukaiona timu ya wataalamu wa kutumia mbwa katika majengo yetu ambao wamealikwa kutembelea mojawapo ya mipango yetu. Kwa vile unaweza kukosa kujua ni aina gani ya mbwa unayemuona katika Howard Center, ni bora kuongea na mshikaji kabla kushirikiana na mnyama. Tafadhali elewa kwamba wengi wa wanyama hawa wako na mtu wao kwa sababu inayohusiana na ulemavu, hivyo ni muhimu kutomsumbua mnyama kwa kutoa sauti, kumpatia chakula, au kujaribu kumbembeleza.

NJIA YA UTUNZAJI WA ZIADA (CARE PATHWAY)

Kuna nyakati ambapo inaweza kuwa muhimu kwetu kukupa utunzaji na uangalizi wa ziada. Tunaita utunzaji huu wa ziada "njia ya utunzaji wa ziada (Pathway)", na unalenga kusaidia usalama wako unapofanya kazi ya kujenga njia ya kuwa na matumaini.

Kupitia njia yetu ya utunzaji wa ziada, tunatoa msaada wa ziada ili kusaidia watu walio katika hatari kubwa ya kujiua. Kipindi hiki cha hatari kinaweza kujumuisha au kisijumuishe mawazo ya sasa ya kujiua. Tunajua kUwa kuna hatari kubwa ya kujiua kwa mtu ambaye amepitia mambo kama vile kuruhusiwa kutoka hospitalini hivi karibuni, jaribio la hivi karibuni la kujiua au hali zingine za maisha. tunaamini kwa dhati kuwa matibabu na msaada vinaweza kukusaidia kuunda mabadiliko ambayo yana tija kwako.

Haya hapa ni mambo ya kutarajia Kutoka kwa utunzaji wa ziada unaotolewa kupitia njia yetu ya utunzaji wa ziada:

- Tutashirikiana kuunda mpango utakaosaidia usalama wako. Hii kwa kawaida huitwa mpango wa usalama.
- Ikiwa tuna wasiwasi kuhusu usalama wako kwa sababu hatujaweza kutagusana nawe, tutawasiliana nawe ili kuhakikisha kuwa uko sawa.
- Wakati watu wanapokuwa na mawazo au tabia za kutaka kujiua, ni muhimu kuwa matibabu na msaada vishughulikie moja kwa moja masuala hayo kabla ya kushughulikia masuala mengine. Tungependa kuwa na uhakika kuwa matibabu na huduma za utunzaji ulizo nazo zinalenga katika kuhakikisha kuwa uko salama nyumbani kwako na kwenye jamii.

HAKI ZA MTEJA NA TAARIFA YA KISHERIA

USIRI WA TAARIFA

Sheria za shirikisho na jimbo zinalinda taarifa yako ya siri. Kuheshimu usiri ni muhimu kwetu. Tutaitumia na kuiweka wazi taarifa yako ya afya kwa ajili ya matibabu, malipo, na shughuli za huduma za afya, kama ilivyoelezwa katika *Notisi yetu ya Shughuli za Faragha*. Hili linajumuisha kutumia na kuweka wazi taarifa ya afya inayokuhusu ili matibabu na huduma utakazozipokea katika shirika ziweze kuidhinishwa na, kulipishwa, na kulipwa na mhusika wa tatu kama vile kampuni ya bima. Taarifa kuhusu matumizi ya mabaya ya Pombe na dawa za kulevya imelindwa na 42 CFR sehemu ya 2 na haiwezi kutolewa au kuwekwa wazi bila idhini yako maalum ya maandishi isipokuwa kama imeruhusiwa vinginevyo na kanuni.

Unashauriwa kwamba chini ya hali fulani za kisheria, kama zifuatazo, taarifa kukuhusu wewe au familia yako inaweza kutolewa bila idhini yako:

- Tumepewa mamlaka na sheria ya Vermont kuripoti matukio kamili au tuhuma za unyanyasaji, kutelekezwa au dhuluma inayowahusu watoto na watu wazima walio hatarini.
- Tunatakiwa kuchukua hatua mwafaka ikiwa uko katika hatari ya kujidhuru mwenyewe, wengine, au umma kwa jumla.
- Tunayo haki ya kuweka wazi tishio la kuaminika la vurugu au madhara lililosababishiwa waathiriwa wanaoweza kutambuliwa, au watu wote kwa ujumla ikiwa ni pamoja na watu au maeneo ya mali.
- Wakati mwingine, huenda tukatakiwa kutii amri ya koti inayotuamuru kutoa ushahidi au kutoa rekodi.
- Tutaiweka wazi taarifa ya afya kukuhusu wewe tutakapohitajika kufanya hivyo na sheria za shirikisho, jimbo, au mtaa.

HAKI ZA WATEJA NA FAMILIA

Lengo la Howard Center ni kutoa huduma na matibabu katika mazingira yaliyo na kizuizi kidogo sana yanayopatikana kwa njia ambayo inaleta jibu na mwafaka kwa sifa zako za kipekee, mahitaji, matamanio, na uwezo.

- Una haki ya kushughulikiwa kwa hadhi na heshima nyakati zote unapopokea huduma. Una haki ya kupata huduma ya kutosha ya kiutu na matibabu.
- Una haki ya kupata huduma na msaada bila kuzingatia utokako, dini, jinsia, kabila, umri, mwelekeo wa kijinsia, au hali yako ya HIV.
- Una haki ya kufahamishwa kuhusu sera sote za shirika zinazoathiri kipindi chako cha matibabu au kupokea huduma. Tafadhali muulize mtoaji wako wa huduma kuhusu taarifa zaidi kuhusu sera mahususi za shirika.
- Una haki ya kufahamishwa kuhusu wasifu wa mtoaji wako wa huduma na kufuzu. Wataalamu wa kiakili waliopewa leseni na wamo katika orodha watapeana wasifu wao na nakala za kufuzu kwako sio zaidi ya mara yao ya tatu ya kukutana nawe. Wasifu na nakala za kufuzu za wafanyakazi wengine wote wa huduma ya moja kwa moja zitatolewa kwako utakapoomba.
- Una haki ya kupokea taarifa kuhusu kigezo cha ustahiki na vipaumbele vya ufadhili, huduma zilizopo, mipango na watoa huduma, miongozo ya shughuli, shughuli za usimamizi, taratibu za kuwasilisha malalamiko na rufaa.
- Una haki ya kuchagua kiwango chako cha ushiriki katika kutengeneza mpango wa kibinafsi

wa matibabu au wa usaidizi ambao unaweza kujumuisha watu wengine na mashirika/mifumo kama unavyopendelea, na kukagua mipango na rekodi kama hizo.

- Una haki ya kutoa idhini ya baada ya kufahamishwa na kushiriki katika maamuzi ambayo yataweka malengo yako ya matibabu/huduma, ikiwa ni pamoja na kueleza mapendeleo yako kuhusu meneja wa huduma aliyechaguliwa, mtaalamu wa tiba, au mtoa huduma mwingine.
- Una haki ya kuchagua huduma katika Howard Center, au mahali pengine. Hata hivyo, kampuni yako ya bima ya afya inaweza kulipia tu huduma ambazo zimetolewa na watoa huduma ambao wameandikishwa kwenye mpango wako wa afya.
- Wakati wa usajili, au wakati wowote wakati wa huduma, unaweza kuanzisha majadiliano na mtoa huduma wako ili kueleza mapendeleo yako kuhusu utoaji wa huduma, kutolewa kwa maelezo, huduma zinazotolewa kwa wakati mmoja, kujua wanachama wa timu yako ya utoaji huduma, na kuhusika katika miradi ya utafiti, ikiwa inatumika.
- Una haki ya kupokea kwa wakati, taarifa inayofaa kukuwezesha kufanya maamuzi.
- Una haki ya faragha. Usiri wako umelindwa na sheria za jimbo na shirikisho isipokuwa kwa hali maalum iliyoruhusiwa au kutakiwa na sheria.
- Una haki ya kukataa dawa au taratibu maalum za matibabu.
- Una haki ya Kupata nakala za rekodi za afya tunazounda na/au kuhifadhi kukuhusu kwa wakati unaofaa, isipokuwa kwa hali fulani. Ombi lako la kupata rekodi litatimizwa bila kucheleweshwa. Una haki za ziada kuhusiana na taarifa yako ya afya zilizoelezwa katika *Notisi ya Shughuli za faragha*.
- Una haki ya ulinzi wote wa kisheria na mchakato wa hali kama mgonjwa asiyelazwa na mgonjwa wa kulazwa, yote kwa hiari au bila hiari, kama ilivyoelezwa chini ya sheria ya Vermont.
- Una haki ya kufikia au kupewa upendekezo kwa taasisi za kisheria kwa uwakilishaji ufaao.
- Una haki ya kufikia au kupewa upendekezo kwa huduma za kujisaidia na msaada wa utetezi.
- Una haki ya kufanya uchunguzi kuhusu madai ya ukiukaji wowote wa haki zako bila kupoteza ufikiaji wa huduma.

- Mtoto au kijana aliye na usumbufu kali wa hisia kama ilivyoelezwa na SHERIA 264 anayehitaji huduma za zaidi ya shirika moja ana haki ya kuundwa kwa Mpangilio Ulioratibishwa wa Huduma kupitia kwa mchakato wa kupanga wa timu yao ya matibabu. Iwapo wewe kama mzazi au mlezi hauridhishwi na uratibu wa huduma, unaweza kukata rufaa chini ya SHERIA 264 kupitia kwa Shirikia la Huduma za Kibinadamu.

Kwa kuongezea haki hizi, washiriki wa baadhi ya mpango huenda wakawa na haki zaidi au haki kuelezwa kwa njia tofauti. Wateja hufahamishwa kuhusu haki zao kila mwaka au mara nyingi kama inavyotakiwa na Jimbo au idara zingine tawala au za udhibiti.

Haki hizi hazimhitahji mtaalamu yeyote wa afya, afya ya kiakili, au huduma kutoa matibabu kinyume na maoni ya mtaalamu kama huyo kama matibabu yamezidi kiwango cha ujuzi cha mtaalamu au huduma imeonekana kuwa hatari kwa ustawi wa mtu binafsi au uko juu ya rasilimali za kifedha za shirika.

Hakuna moja ya haki zilizo hapo juu itakayozuia programu kupunguza au kuondoa kabisa huduma kwa mtu ambaye utoaji wa matibabu mwafaka au huduma haiwezekani kutokana na sababu za mtu kukataa kuridhia au kushirikiana na huduma zinazowezekana alizopewa na msaada.

WAJIBU WA WATEJA NA FAMILIA

Huduma zina ufanisi tu wakati kuna ushirikiano baina ya mteja na mtoaji huduma. Wahusika wote wanahitajika kujitolea kabisa kuyafikia malengo ya matibabu au huduma. Tunawaomba wateja wote kujitolea kwa yafuatayo:

- Kushiriki kila mara katika matibabu au huduma
- Kuhudhuria kila mara ziara zilizopangwa au miadi
- Malipo kwa wakati wa huduma wakati malipo ya moja kwa moja yamekubalianwa
- Kusuluisha tofauti kwa njia inayokubalika
- Vitisho vya kimwili au vya maneno, tabia ya fujo au uharibifu hairuhusiwi
- Silaha hazijaruhusiwa katika majengo ya shirika.
- Unahitaji ruhusa iliyotolewa kwa mdomo ya kupiga picha au kurekodi mfanyakazi yeyote wa shirika; wafanyakazi hawapaswi kuwa kwenye picha au rekodi zozote
- Hakuna kuvuta au kutumia bidhaa za tumbaku kumeruhusiwa katika majengo ya shirika
- Hakuna dawa haramu au pombe zimeruhusiwa katika majengo ya shirika

Kama matarajio yaliyo hapo juu hayajafuatwa, shirika lina haki ya kusitisha au kuweka vikwazo kwa huduma. Haki zote au pendeleo ambazo zimewekewa vikwazo au kusimamishwa zinaweza kurejeshwa kwa hiari ya shirika, kulingana na hali ya mtu binafsi na sababu za vikwazo au usimamishaji.

MUHTASARI WA KANUNI ZA MAADILI

Howard Center kimeunda Kanuni za Maadili za kina ambazo kinatarajia wanyikazi wake kuzingatia. Muhtasari wa matarajio ya kimaadili yameelezwa hapa chini.

- Wafanyakazi wa Howard Center wataheshimu na kuzikuza haki za wateja kwa kujitegemea na watawasaidia wateja kutambua na kufafanua malengo yao.
- Wafanyakazi wa Howard Center hawatajihusisha kimakusudi katika tabia ya unyanyasaji au udhalilishaji kwa watu ambao wanawasiliana nao katika kazi zao au kushirikiana nao, kusaidia au kuwezesha ubaguzi usio wa haki kwa misingi ya umri wa mtu, jinsia, rangi, kabila, asili ya kitaifa, dini, mwelekeo wa kijinsia, ulemavu, lugha, au hali ya kijamii na kiuchumi.
- Wafanyakazi wa Howard Center hawatatumia lugha ya madharau kwa njia yoyote ya maandishi au mawasiliano ya maneno.
- Wafanyakazi wa Howard Center hawata jihusisha na mtagusano wa kimwili ambao si wa lazima kimatibabu, na usiozingatia matukio ya kiwewe na wateja.
- Wafanyakazi wa Howard Center watapata ridhaa ya ufahamu ifaayo kwa matibabu au taratibu husika, isipokuwa katika matukio ambayo uwezo wa ridhaa una utata.
- Wafanyakazi wa Howard Center wataeleza huduma inayotolewa na matokeo yoyote ya huduma kama hizo kwa lugha inayoeleweka na mpokezi wa huduma hizo.
- Wafanyakazi wa Howard Center watachukua hatua kuweka mipaka ifaayo wakati haiwezekani au kuna sababu ya kuepuka utangamano wa kijamii au mwingine usio wa kitaalamu na wateja, wanafunzi, wasimamizi, au washiriki wa utafiti. Wakati inawezekana, wafanyakazi wa Howard Center watajitenga na kutibu wateja pale ambapo uhusiano ulioko unaweza kusababisha madhara au pale uhusiano wa kingono ulikuwepo mbeleni.
- Wafanyakazi wa Howard Center watafanya juhudi nzuri ili kupanga huduma katika tukio ambalo huduma za kisaikolojia zimetatizwa na sababu kama vile, ugonjwa, kifo, au upangaji wa upatikanaji.
- Wafanyakazi wa Howard Center hawatawaacha wagonjwa au wateja. Wafanyakazi wa Howard

Center watatamatisha kwa njia ifaayo uhusiano wa kitaalamu itakapokuwa wazi kwamba mgonjwa au mteja haihitaji tena huduma au hafaidiki kutokana na huduma.

- Wafanyakazi wa Howard Center watajadiliana na wateja mapema iwezekanavyo, kuhusu aina ya huduma zinazotarajiwa, ada, vigezo vya ustahiki wa wafanyakazi na usiri.
- Wafanyakazi wa Howard Center wanatakiwa kuripoti unyanyasaji unaoshukiwa wa watoto na watu wazima walio hatarini na tishio la madhara kwa mtu binafsi, watu wengine au watu wote kwa jumla.
- Mapema iwezekanavyo katika uhusiano wa kitaaluma, wafanyakazi wa Howard Center na mteja, au mpokeaji mwingine anayefaa wa huduma, watafikia makubaliano yanayobainisha mipangilio ya bili. Wafanyakazi wa Howard Center na mteja/mlezi watajaza Fomu ya Makubaliano ya Malipo na kujadili vikomo vyovyote vya huduma vinavyoweza kutokea kwa sababu ya ufadhili/bima.
- Wafanyakazi wa Howard Center watafanya utathmini, huduma za utambuzi, au uingiliaji kati wakiwa tu katika muktadha wa uhusiano uliofafanuliwa wa kitaalamu.
- Wafanyakazi wa Howard Center wataepuka kupokea, zaidi ya shukrani za kawaida, zawadi, malipo ya kibinafsi, bidhaa, huduma, au malipo mengine yasiyo ya fedha kutoka kwa wateja.

Toleo zima ya Kanuni za Maadili za Howard Center, ukiwemo muhtasari uliopo hapo juu pamoja na mada, unaweza ukapatikana katika tovuti yetu kwa **www.howardcenter.org**.

MALALAMIKO YA MTUMIAJI NA SERA YA RUFAA NA TARATIBU

Kama mteja wa Howard Center, uko na haki ya kuwasilisha manung'uniko kuhusu huduma unazozipokea. Tunakuhimiza sana kuomba nakala yetu kamili ya *Sera na Taratibu za Nung'uniko na Tetezi*, kwani iko na taarifa ya kina iliyoundwa kukusaidia kwa mchakato huu wote. Ongea na mtoaji wako wa huduma au mhudumu wa meza ya mbele kuomba taarifa zaidi. Kwa urahisi wako, tumeiweka sera kwa muhtasari katika kurasa kadhaa zifuatazo.

MAELEZO

Tathmini Mbaya ya Manufaa: inamaanisha yoyote ya yafuatayo:

- Kukataliwa au uidhinisho mdogo wa huduma iliyoombwa, ikiwa ni pamoja na maamuzi kwa misingi ya aina au kiwango cha huduma, mahitaji ya umuhimu wa kimatibabu, ustahili, muundo, au ufanisi wa huduma iliyo shughulikiwa
- Kupunguzwa, kusimamishwa, au kutamatishwa kwa huduma iliyoidhinishwa hapo awali
- Kukataliwa, kwa yote au sehemu, ya malipo kwa huduma
- Kukosa kutoa huduma kwa wakati ufaao, kama ilivyoelezwa na Shirika ya Huduma za Kibinadamu
- Kukosa kushughulika kwa wakati uliowekwa kuhusiana na kiwangogezi cha usulihishaji wa tetezi na rufaa
- Kukataliwa kwa ombi la mfaidi kupata huduma nje ya mtandao
- Kukataliwa kwa ombi la mfaidi kupinga deni ya kifedha, ikiwa ni pamoja na gharama ya kugawa, malipo ya pamoja, dhamana, mapunguzo, bima za pamoja, na deni nyingine za mfaidi

Rufaa (inahusisha watu walio na Medicaid): Ombi rasmi la maneno au lililoandikwa kutoka kwa mtumiaji kwenda kwa shirika kuangalia upya maamuzi yake ya tathmini mbaya au nung'uniko. **Rufaa iliyoharakisha** ni rufaa ya hali ya dharura ambayo inaweza kuhatarisha vibaya maisha ya mtumiaji; afya; au uwezo wa kufikia, kudumisha, au kurejea tena upeo wa kufanya kazi.

Mwakilishi Aliyeidhinishwa: mtu binafsi, aliyeteuliwa aidha na mteja au aliyeidhinishwa chini ya sheria za jimbo, kushughulika kwa niaba

ya mteja anayepata uamuzi au anayeshughulika na kiwango chochote cha tetezi au mchakato wa rufaa. Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo, mwakilishi aliyeidhinishwa ako na haki zote na majukumu ya mteja anayemwakilisha.

Usikilizwaji wa Kesi kwa Haki: Hii inatumika kwa watu binafsi wenye Medicaid na ni ni mchakato wa kisheria ambao haufanyika mahakamani ambapo mtumiaji na shirika lililoteuliwa kila mmoja huwasilisha upande wake wa hali hiyo kwa afisa mtaalam anayesikiliza kesi hiyo. Kusikizwa kwa haki kunapatikana tu wazi kama chaguo baada ya mtumiaji kutumia kabisa mchakato wa ndani wa Howard Center kuhusiana na uamuzi mbaya wa tathmini.

Tetezi: maelezo ya maneno au yaliyoandikwa ya kutoridhika kwa mtumiaji kuhusu jambo lolote mbali na uamuzi mbaya wa tathmini.

Uchunguzi wa Tetezi: Kupitiwa kwa ndani kwa ndani kwa mchakato wa kufanya maamuzi ya tetezi na mtu asiyehusika moja kwa moja asiyeengemea upande mmoja ndani ya Howard Center.

SERA

Nung'uniko au rufaa zitapitiwa ifaavyo, na kuzingatiwa kwa wakati ufaao. Wateja, na/walezi, kama inahusika, watafahamishwa kuhusu sera na taratibu za malalamiko, nung'uniko na rufaa za shirika watakapochukuliwa na baadaye kila mwaka, au katika mzunguko tofauti kama mikataba maalum inamuru. Sera na taratibu hizo zitabadikwa katika maeneo ya huduma, na kwenye tovuti ya shirika. Kwa kuongezea, wahudumu wote watafundishwa kuhusu nung'uniko ya mtumiaji, tetezi, na sera ya rufaa na taratibu watakapoajiriwa na kila baada ya miaka miwili baadaye. Mtu yeyote anayeanzisha au kufuatilia malalamiko, tetezi au rufaa atakuwa huru kutokana na aina yoyote ya ulipizaji kizazi au ubaguzi. Maswali yoyote kuhusu sera hii au taratibu husiani yanafaa kuelekezwa kwa Afisa Anayehakikisha Uutiifu wa Sheria wa Howard Center. Kuna wawakilishi zaidi wanne wa shirika kuhakikisha uzingatiaji wa sera hii. Afisa Anayehakikisha Utiifu wa Sheria atahudumu kama mratibu wa malalamiko na rufaa wa Howard Center kwa ujumla na anawajibu wa kuhakikisha uchakataji na usuluhishwaji kwa wakati ufaao wa malalamiko na rufaa zote. Majadiliano yote yanayozunguka mchakato

wa maamuzi ya tetezi au rufaa yatawekwa kwa siri kutoka kwa umma kwa jumla au watu wasiohuika moja kwa moja, isipokuwa kama imeombwa vinginevyo na mteja.

Kama unaamini kwamba ufaragha wako umekiukwa, unaweza kuwasilisha malalamiko kwa shirika au kwa Katibu wa Shirika la Vermont wa Huduma za Kibinadamu. Ili kuwasilisha malalamiko kwa shirika, wasiliana na Laini ya Uzingatiaji kupitia kwa simu kwa nambari iliyoandikwa hapa chini. Tafadhali kumbuka kwamba malalamiko ya ufaragha yanashughulikiwa kama inavyotakikana chini ya sheria za shirikisho na hayashughulikiwi kupitia mchakato wa tetezi wa shirika.

Wateja wa Mpango wa Park Street na Mpango wa Makazi ya Mpito wako na haki zaidi iliyoandikwa katika sera ya shirika katika Sheria ya Kumaliza Ubakaji katika Jela (Prison Rape Elimination Act, PREA). Fomu ya malalamiko ya PREA inapatikana katika tovuti ya **www.howardcenter.org**.

Muda na mahitaji maalumu ya idara huenda zikatofutiana kutegemea mpango ambao nung'uniko, tetezi, au rufaa imetokea. Mwakilishi aliyeteuliwa wa tetezi na rufaa atakuwa na wajibu wa kupitia upya na uzingatiaji wa mahitaji tofauti ya kiidara, wakati ambapo hayajaelezwa katika sera hii.

Kwa wakati wowote mhudumu au mteja anaweza kuwasiliana na Laini ya Uzingatiaji kwa kupiga simu kwa 802-488-7195 ili kuacha ujumbe wa sauti wa kisiri. Hili linaweza kuwa bila jina. Vinginevyo, wateja wanaweza kutuma maombi yoyote ya malalamiko au rufaa kwa clientG&A@howardcenter.org. Simu na barua pepe zote zitatambuliwa na kukaguliwa.

Nakala za sera kamili ya shirika na taratibu zipo kwa ajili ya kila mteja atakapoziomba.

OFISI YA UDHIBITI WA KITAALUMA – MWENENDO NA MCHAKATO WA MALALAMIKO

Ofisi ya Udhibiti wa Kitaaluma wa Katibu wa Jimbo la Vermont inatoa leseni, vyeti, na usajili wa Vermont kwa zaidi ya madaktari na biashara 55,000.

Kila taaluma au kazi imeongozwa na sheria zinazoeleza mwenendo wa kitaaluma. Ikiwa hii inatumika kwa mtoa huduma wako aliyeidhinishwa/aliye kwenye orodha katika Howard Center, atakupa

nakala ya Fomu yake ya Ufichuzi na sheria husika. Unaweza kupata nakala za sheria maalum katika tovuti ya Ofisi ya Katibu wa Jimbo ya Udhibiti wa Taaluma kwenye kwenye https://sos.vermont.gov/opr/.

Wateja ambao wangetaka kuwasilisha malalamiko wanaweza kufanya hivyo katika tovuti ya Ofisi ya Udhibiti wa Taaluma kwa kutembelea https://sos.vermont.gov/opr/complaints-conduct-discipline/. Kwa taarifa zaidi unaweza kuwasiliana na Ofisi ya Udhibiti wa Taaluma kwa kuiandikia barua au kupiga simu:

Office of Professional Regulation
89 Main Street, 3rd Floor
Montpelier, VT 05620-3402
802-828-1505

Malalamiko yanapopokelewa, mapitio ya kiusimamizi uamua kama masuala yaliyoimbuliwa yameshughulikiwa na sheria husika ya mwenendo wa kitaaluma. Kama ni hivyo, kamati inateuliwa ili kuchunguza, kukusanya taarifa, na kupendekeza hatua au kufungwa kwa idara simamizi inyofaa.

Uchunguzi wote wa malalamiko ni za siri. Ikiwa uchunguzi utamalizia kwa uamuzi wa hatua ya kinidhamu kinyume na leseni ya mtaalamu na uwezo wa kufanya kazi, jina la mmiliki wa leseni hio sasa litawekwa hadharani kwa umma.

Hatua ya kinidhamu kupitia kwa Ofisi ya Udhibiti wa Taaluma inaanzia kutoka kwa Kuonya hadi kufutiliwa mbali kwa leseni, lakini haihusishi fidia ya kifedha, ikiwa na yaliyotegwa. Malipo ya kifedha yanaweza kufuatiliwa kupitia kwa wakili wa kibinfsi, koti za madai madogo, au kwa Kitengo cha Ulinzi wa Mtumiaji katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

FOMU YA USHAURI KWA MTEJA
(nakala ya rejeleo pekee)

HOWARD CENTER
Help is here.

Ushauri kwa Mteja

* Uamuzi wako wa kutumia huduma zetu ni wa hiari.
* Huduma za Kituo cha Howard ni juhudi za ushirikiano baina ya mteja na mtoaji huduma. Wakati tukiamini kwamba huduma zetu zitakuwa za manufaa kwako, hakuna uhakikisho kuhusu matokeo ya matibabu, Utathmini, au msaada.
* Baadhi ya Mipango huenda zikatumia utaalamu au mbinu katika kipindi cha matibabu kama vile kutafakari, yoga, au picha iliyoongozwa. Mtoaji wako wa huduma atajadiliana nawe kwa kina iwapo utakuwa wa kupokea yeyote ya huduma hizi.

Uthibitisho wa mteja wa ufichuzi

Nimefahamishwa katika Kituo cha Howard ikijumuisha:

1. Ujumbe na maadili
2. Saa za Kufanya kazi, zikiwemo Huduma za Mzozo
3. Jinsi ya Kuzifikia Huduma na Muundo wa Shirika
4. Mchango wa Mtumiaji
5. Ulipiaji wa Huduma
6. Utegenezaji wa Mazingira Salama
7. Usiri wa Taarifa
8. Haki za Wateja na Familia
9. Wajibu ya Wateja na Familia
10. Muhtasari wa Kanuni za Maadili
11. Malalamiko ya Mtumiaji, Tetezi na Sera ya Rufaa na Taratibu
12. Ofisi ya Udhibiti wa Taaluma– Mwenendo na Mchakato wa Malalamiko
13. Wasifu wa Mtoaji wangu wa Huduma na Kufuzu
14. Njia za Eneo za Kutorokea wakati wa Dharura na Pahali vitu vya kuzima moto zilipo
15. Notisi ya Shughuli za Faragha

Nimefahamishwa kuhusu taarifa ya hapo juu na kuielewa na kuridhia yaliyomo.

Mteja/Mzazi/Mlezi (tafadhali bainisha): ________________________ Tarehe: ________

Mteja/Mzazi/Mlezi (tafadhali bainisha): ________________________ Tarehe: ________

USHIRIKISHAJI WA JAMII NA UPANGAJI WA MIPANGO

Idara ya **Uanuai, Usawa na Ujumuishaji** ya Howard Center inatekeleza mipango muhimu ndani na nje ya jamii ya Howard Center ambayo inaendana na mahitaji ya jamii yetu inayobadilika kila mara. Tunawajibikia ukuaji na maendeleo endelevu, kushughulikia madhara ya jamii, kukuza urejeshaji wa ustawi na kujenga utamaduni wa heshima na kutegemeana kwa kila mtu. Tunawajibikia pia kwa usawa ukuzaji wa uwakilishi na kutoa msaada endelevu kwa watu wetu wote, ikijumuisha, lakini sio tu, watu wa rangi tofauti, wamarekani wageni, watu waliobadili jinsia na watu wa uwili jinsia na watu wenye ulemavu.

JE UNGEPENDA KUJISAJILI KUPIGA KURA?

Kama haujasajiliwa kupiga kura na ungependa usaidizi, tafadhali ongea na mtoa huduma wako au mfanyakazi wa meza ya mbele ili kupata fomu ya usajili. Ili kustahiki kupiga kura katika Vermont, lazima:

1. uwe raia wa Marekani;
2. uwe mkaazi wa Vermont na mkaazi wa mji ambao unaomba uongezwe katika orodha;(AU uwe mwanajeshi au mpiga kura wa nje ya nchi aliyehitimu kulingana na Sheria ya Kupiga Kura ya Wasiokuwepo ya ushirika wa Wanajeshi na Raia walioko Nje ya Nchi ambao makao yao ya mwisho katika Marekani mara kabla ya kwenda nje ya nchi yalikuwa mjini Vermont);
3. uchukue, au uwe ulichukua awali, Kiapo Cha Mpiga Kura; na
4. uwe na umri wa miaka 18 au zaidi au uwe na umri wa mika 18 wakati au kabla ya siku ya uchaguzi.

HOWARD CENTER presents
THE MARNA AND STEPHEN WISE TULIN
COMMUNITY EDUCATION SERIES
FREE AND OPEN TO THE PUBLIC

Katika mwaka wa 2015, Howard Center ilianza kutoa **mfululizo wa masomo ya elimu ya jamii bila malipo na ambayo yangeweza kufikiwa na umma** kama sehemu ya dhamira na huduma yetu kwa jamii ili kusaidia kuelimisha, kufahamisha, kupunguza unyanyapaa na kuongeza uelewa kuhusu mada mbalimbali zinazohusiana na afya

Tunatambua kuwa watu wakielewa vizuri zaidi kuhusu changamoto za kiafya, tunaweza kusaidia kuunda jamii yenye huruma na inayohusika zaidi. Mawasilisho yanarekodiwa kwa video na yanapatikana kwenye www.howardcenter.org.

Tafadhali jiunge nasi katika hafla zetu zozote za elimu ya jamii. Kwa taarifa zaidi, tembelea howardcenter.org.

Howard Center Arts Collective ni kundi la wasanii ambao ni watu wazima wa viwango vyote vya ujuzi ambao wamepitia matatizo ya ugonjwa wa akili na/au changamoto za matumizi ya dawa za kulevya, wao binafsi, na familia au marafiki, au katika kazi zao. Tunashirikiana ili kuhakikisha kuwa wasanii wetu wana fursa za kuwasiliana na watu wengine, kuunda na kuonyesha kazi zao za sanaa. Tunathamini uwezo wa mabadiliko wa mchakato wa ubunifu katika kiwango cha kibinafsi, kijamii na kimfumo, na tunakubali kuwa tuna nguvu zaidi wakati maoni ya kila mmoja yanazingatiwa.

Jalada la brosha, angalia watu waliotambuliwa kwa michango yao kwenye ukurasa wa 2.

Ikiwa unatafuta jumuiya inayostawi ili usaidie na ukuze ubunifu wako, tutumie barua pepe kwa artscollective@howardcenter.org.

USAIDIZI UKO HAPA.

We respect **WOMEN, MEN** and **NON-BINARY PEOPLE** • We value **BLACK LIVES** • We stand with our **LGBTQIA+ COMMUNITY MEMBERS** • We celebrate **CHILDREN** • We stand with **IMMIGRANTS**, **REFUGEES**, **INDIGENOUS PEOPLES**, and **PEOPLE OF ALL FAITHS and ETHNICITIES** • We support **INDIVIDUALS** and **FAMILIES** challenged by mental health, substance use, and developmental disabilities.

*We stand with our **COMMUNITY**.*

HATE HAS NO BUSINESS HERE.
All Are Welcome Here.

الجميع مرحب به هنا • Tất cả đều được chào đón ở đây

Tout le monde est le bienvenu ici • အားလုံးကို ဒီနေရာမှ ကြိုဆိုပါတယ်

Dadka kulushoo ha dhawaatheen • *Ovdje su svi dobrodošli*

歡迎各位 • **Dhammaan waa la soo dhaweynayaa**

Wote wanakubaliwa hapa • Todos son bienvenidos aquí

Сви су добродошли овде • མི་ཚང་མ་ཕེབས་པར་དགའ་བསུ་ཡོད།

सबै जनालाई यहाँ स्वागत छ।

UNITED WAY Northwest Vermont

Vermont Care Partners — Center of Excellence

HOWARD CENTER
Help is here.
TANGU 1865

Ilisasishwa Januari 2025